Hapa kwetu nyumbani ni sharti tujikumbushe mapambano ambayo yalisababisha wilaya yetu kutengwa na ilianza na maandamano yaliyofanywa na Caunt Samuel Teleki mwaka 1888. Maandamano mengine yalifuatia mwaka 1898na 1901, 1910, 1918 hadi miaka ya 1950 na utawala wa Muingereza ukapingwa vikali. Kodi ya lazima ya vibanda iliyoanzishwa na wakoloni kwa mfumo wa mifugo ilionekana kama uvamizi na hapo ndipo desturi ya wizi wa mifugo ilianza kwani wale waliopokonywa mifugo wao ilibidi waende kwa majirani kuiba mifugo ili kufidia mifugo walioibwa.

Hivyo basi tunawakumbuka na kuwaenzi mashujaa wetu, Jenerali Ebei, Jenerali

Nathura Aunomeri, Echan Ebei, Nadima, wakongwe wa itikadi (Ngimurok) Lokorijem, Kokoi Looel, Lobwin Aseneng'moe, hao wakiwa ni baadhi tu ya mashujaa waliokaidi na kukataa kuutambua utawala wa Mkoloni na kuifanya Turkana eneo la mashambulizi ya kijeshi. Ili kuwapa heshima na kuwaenzi mashujaa hawa tutaandika majina yao katika taasisi za umma katika kaunti yetu.

### **Mabibi na Mabwana,**

Nilipochukua uongozi kama Gavana mwaka 2013, Nilirithi Kaunti hii kutoka kwa Serikali ya Wilaya iliyokuwa na changamoto si haba. Changamoto hizo zilikuwa ni Pamoja na uhaba mkubwa wa maji, miundomsingi ya afya iliyodorora na nyingine nyingi.

Katika kipindi cha miaka 10 ya utawala wangu, tumepiga hatua kubwa kukabiliana na changamoto hizo kwa kuwekeza katika miradi ya maendeleo ambayo imewapa wakaazi matumaini na kuweka mzingi wa wa mabadiliko katika Kaunti yetu. Tumewekeza katika kupeleka serikali karibu na nyumbani kwa kuanzisha miradi ambayo imeboresha hali ya maisha ya atu wetu na kujenga ushirikiano imara na majirani zetu, washirika wa kimaendeleo na sekta ya kibinafsi.

Licha ya uwekezaji wa jumla ya Shilingi Bilioni 154.3 ambao umefanywa na serikali ya Kaunti tangu mwaka 2013 katika sekta muhimu kufikia sasa hii hajatosha kuileta Kaunti hii kuwa kiwango saw ana Kaunti nyingine nchini Kenya.

Makadirio katika Mpango wetu wa Maendeleo (County Integrated Development Plan (CIDP) yanaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita zaidi ya Shilingi Bilioni 30 zingehitajika kila mwaka ili Turkana iweze kuwa sawa na Kaunti nyingine zilizoendelea humu nchini.

Katika juhudi za kuziba pengo hili la rasilimali, utawala wangu umeimarisha ushirikiano na mashirika ya kimaendeleo, sekta ya kibinafsi na mashirika ya kijamii. Chini ya utawala wangu kupitia Mpango wa Ustawi wa Kiuchumi na Kijamii wa Kalobeyei tuliweza kushirikisha shilingi Bilioni 58 katika kipindi cha miaka 10 iliyopita ambapo Shilingi Bilioni 44 ziliwanufaisha wakimbizi ambapo Shilingi Bilioni 14 ziliwanufaisha Wenyeji wa Turkana. Hii ni kupitia ushirikiano katika kuratibu mipango, hasa katika sekta muhimu za Aya, Maji, Utoshelevu wa Chakula na Lisheboru, na kuweka Amani, maongozi na ustawi wa kibiashara

Katika sekta ya Huduma za Afya na Usafi, Serikali yangu imepiga hatua kubwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kupitia uratibu kabambe wa mipango, kutenga rasilimali na kujitolea kwa wahudumu wetu wa Afya kufanya kazi kwa bidii.

Taasisi zetu za afya zimeongezeka kutoka 78 mwaka 2013 hadi taasisi 288 kwa sasana zinaendelea kuongezeka. Ongezeko la taasisi hizi limepunguza kwa kiwango kikubwa umbali wa taasisi moja hadi nyingine kutoka Kilomita 55 mwaka 2013 hadi kilomita 15 leo hii. Idadi ya vitanda vya wagonja imeongezeka hadi vitanda 1400 kutoka vitanda 300 mwaka 2013.

Idadi ya wahudumu wetu wa afya sasa ni 1800 kutoka 272 mwaka 2013. Zaidi yah apo tumesajili wahudumu wa afya ya jamii wa kujitolea 2068 kuboresha huduma za afya mashinani. Uwiano wa Daktari kwa mgonjwa umepungua kutoka Daktari mmoja kwa wagonjwa 70,000 mwaka 2013 hadi Daktari mmoja kwa wagonjwa 20,000 mwaka 2021, huku uwiano wa muuguzi kwa mgonjwa ukipungua kutoka muuguzi mmoja kwa wagonjwa 5,200 mwaka 2013 hadi muuguzi mmoja kwa wagonjwa 232 wakati huu.

Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Lodwar imeshuhudia ustawi mkubwa wa miundimsingi katika juhudi za kuipandisha hadhi kufikia kiwango cha Level 5. Juhudi hizi ni pamoja na kuweka mtambo wa kutengeneza Gesi ya Oxygen , ujenzi wa chumba cha kuhifadhi maiti chenye uwezo wa kuhifadhi miili 66 na ujenzi wa tanuri ya kuteketeza taka za kimatibabu ya gharama ya shilingi Milioni 20. Mashine ya Citi Scan, Ultra Sound, Gene X-pet, Jengo la vitanda 12 vya ICU, kitengo cha matibabu ya dharura na ajali, chumba cha upasuaji na kitengo cha usafishaji damu (Dialysis) na nyumba za madaktari. Ustawi huu umeboresha huduma na kuhakikisha rufaa za nje ya kaunti zinapungua kwa asilimia 80

Tumeweka mtambo wa jenereta kushughulikia swala la kupotea kwa nguvu za umeme huku mipango ikifanywa kushughulikia tatizo la maji la mara kwa mara.

Ili kuongeza uwezo wa kukabiliana na mikasa ya dharura, Serikali ya Kaunti imeongeza idadi ya Magari ya kubeba wagonjwa kutoka manne mwaka 2013 hadi 28 wakati huu. Katika juhudi za kupunguza rufaa kutoka Kaunti Ndogo hadi Hospitali Kuu ya Lodwar, tumejenga na kuweka vifaa vyumba vitano vya upasuaji katika vituo vya afya vya Lopiding', Katilu, Elelea, Lorugum na Lokitaung. Chumba cha upasuaji wa macho cha Lokitaung kilichoinduliwa mwaka jana ndicho cha pili kwa ubora wa vifaa katika Kaunti na sio tu kinawanufaisha raia wa Turkana bali pia wakaaji wa Dassanach na Nyangatom nchini Ethiopia.

Utawala wangu umeweka msitari wa mbele usambazaji wa vifaa vya matibabu na teknolojia ili kuhakikisha matokeo bora ya kiafya. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Shilingi Bilioni 2.5 zimewekezwa katika kununua madawa kwa taasisi zote za kaunti

Shughuli zetu za chanjo zimeimarika kutoka asilimia 45 nukta 2 mwaka 2013 hadi ailimia 84 nukta 2 mwaka 2021; huku kiwango cha maambukizi ya Virusi

vya UKIMWI yakipungua kutoka asilimia 6 nukta 9 mwaka 2013 hadi asilimia 2 nukta 2 mwaka 2021. Maambukizi ya maradhi ya Malaria nayo yamepungua kutoka asilimia 40 hadi asilimia 3 nazo huduma za uzazi zikiongezeka kutoka asilimia 25 nukta 2 hadi asilimia 65 nukta 1

Huduma za kliniki za kina mama waja-wazito zimeongezeka licha ya changamoto ya wengine kukosa kliniki kutokana na ukosefu wa hamasisho. Utumizi wa huduma hizi angalau kliniki nne za kwanza umeongezeka kutoka asilimia 33 nukta 4 hadi asilimia 66 nukta 5.

Licha ya ufanisi huu wote, mengi yanahitaji kufanywa ili kuboresha hali ya lishe katika kaunti. Hali ya utapiamlo duniani ni kati ya asilimia 15 na 30 na ipo haja ya elimu ya afya kutolewa kwa kina mama ili kuboresha upatikanaji wa virutubisho vya lishe katika taasisi zetu za afya na vituo vya masomo ya chekechea na kuwekeza katika utoshelevu wa chakula na lishebora.

Sheria ya Huduma za Afya ya Jamii ya Turkana iliyobuniwa mwaka 2018 ilianzisha Vituo vha Afya ya Jamii na kuwezesha kuteuliwa kwa Wahudumu wa Afya ya Jamii wa kujitolea. Tumewapa wahudumu 2068 wa Afya wa kujitolea mafunzo kuhusu ukaguzi wa kimsingi na matibabu na hii imeimarisha kuzuia magonjwa na haja ya kwenda kutafuta matibabu.

Janga la Covid-19 lilitupatia mihani mkubwa kama kaunti. Utawala wangu ulianzisha hazina ya Covid-19, tukanunua vifaa maalum, tukawashirikisha washirika wetu wa kimaendeleo kusaidia kuzuia na kudhibiti janga hilo. Kwa ujumla tuliweza kupima zaidi ya watu 900,000. Wale walioambukizwa kufikia sasa ni 2,647 na tumerekodi huku 2578 wakipona na kurekodi vifo 69. Kiwango cha maambukizi katika kaunti yetu sasa ni asilimia 4. Ushirikiano wetu na serikali ya kitaifa katika mpango wa chanjo za Covid-19 umeleta mafanikio ambapo Zaidi ya watu 107,000 wamechanjwa huku 80,036 wakiwa wamepata chanjo kamili ya Covid-19. Nawasihi wakaazi kuhakikisha wamepata chanjo ya Covid, hii ni kwa sababu hatari ya maambukizi na kuibuka kwa aina mpya za ugonjwa huo bado iko juu.

### **Mabibi na Mabwana,**

Katika sekta ya maji tumeongeza idadi ya visima katika kaunti yetu kutoka 511 mwaka 2013 hadi 1,967 wakati huu. Idadi ya mifumo ya pampu za maji kutumia umeme wa miale ya jua imeongezeka kutoka 200 mwaka 2013 hadi 564 saa hii. Tumechimba silanga za maji na kuongeza idadi kutoka 64 mwaka 2013 hadi 230 wakati huu.

Uwekezaji katika miradi hii ya maji umepunguza umbali ambao wakaazi wamekuwa wakitembea kutafuta maji kutoka kilomita 12 hadi kilomita 5 huku idadi ya familia zinazopata maji safi ikiongezeka kutoka 33,237 mwaka 2013 hadi 97,600 kwa sasa. Kupatikana kwa maji hata hivyo kunakumbwa

na changamoto ya ukame wa mara kwa mara unaosababisha vyanzo vya maji vya chini ya arhi kukauka, mito ya maji ya chini ya ardhi iliyo mbali Zaidi na kuvunjika kwa pampu za maji za mkono hivyo kuwafanya wafugaji kutembea mwendo mrefu kutafuta maji.

Sheria ya Maji ya Turkana ya mwaka 2019 iliwezesha kubumiwa kwa mifumo ya usimamizi wa maji zikiwemo: Kamati ya Ushirikishi wa Sekta ya Maji Kaunti ya Turkana, Kampuni ya Maji ya Turkana Mjini na Kampuni ya Maji ya Turkana Mashinani. Utendajikazi wa Hazina ya Maji na Mifumo ya Usimamizi wa Maji inatarajiwa kuboresha utoaji wa huduma za maji na usimamizi wa miundomsingi ya maji katika kaunti.

### **Wakaazi wenzangu,**

Katika Sekta ya Ardhi, Kawi, Nyumba na usimamizi wa sehemu za miji, Serikali yangu imepandisha hadhi Mji wa Lodwar na kuwa Manispaa ili kuharakisha ustawi wa miundombinu ya mijini, kuboresha utoaji huduma, kuongeza mapato na kuvutia uwekezaji. Haya yote yatabuni mazingira bora kwa biashara na kuweka utaratibu murua katika sekta ya usafiri na hivyo kupandisha hadhi na thamani ya mji wa Lodwar.

Pia tuko katika harakati ya kupandisha hadhi Mji wa Kakuma/Kalobeyi. Vile vile vituo vya kibiashara vya Kalokol, Lokichar na Lokichoggio vinapangiwa kuidhinishwa kuwa miji.

Ili kukabiliana na changamoto ya uzoaji wa taka katika miji yetu, tumebuni majaa katika vitongoji vya miji ya Lodwar, Kalokol, Kakuma, Lokichoggio, Katilu na Lokichar. Tunashirikiana na Shirika la Ujerumani la GIZ kuweka kituo cha kusafisha majitaka.

Serikali ya Kaunti ina huduma za zimamoto za kukabiliana na mkasa wowote wa moto unapozuka katika Manispaa ya Lodwar. Katika kipindi cha mwaka huu cha matumizi ya fedha za serikali, idara hiyo imeshughulikia na kuzima visa 25 vya moto ambao ungeleta hasara kubwa ya maafa na kuteketea kwa mali ya jamii.

Utawala wangu una nia ya kuwawezesha wakaazi wa Manispaa ya Lodwar kupitia kuhalalisha umiliki wa ardhi. Tunanuia kushughulikia hati 7,200 za umiliki wa ardhi na kuharakisha usajili wa ardhi ya jamii ili jamii ziweze kubaini kitengo chao cha usajili wa ardhi. Tunasubiri maafisa kutoka Idara ya Usorovea na Tume ya Ardhi nchini kukamilisha utoaji wa hati miliki hizo za ardhi. Hii itasaidia kupunguza migogoro inayohusiana na ardhi na kurahisisha upatikanaji wa mikopo miongoni mwa wakaazi.

## **Mabibi na Mwabwana,**

Kupitia ushirikiano wa kimkakati, nina furaha kuripoti kwamba Serikali ya Kaunti ya Turkana na Wizara ya Ulinzi hivi majuzi zilitia saini Makubaliano ya Mfumo wa ugawaji wa ardhi kwa matumizi ya kijeshi katika maeneo tofauti ya kaunti..

Kuambatana na Sheria ya Ardhi ya Jamii, jamii imetoa idhini ya kutenga kutenga ardhi huko katika wadi za Kanamkemar huko Kaputir, Kapedo/Napeitom, Lapur, Kibish, Lokichoggio, Nanam na Letea; na kutoa ruhusa ya matumizi ya Hekta 50,000 za ardhi huko Kapedo/Napeitom kwa mafunzo ya kijeshi endapo itatokea haja.

Mikataba hiyo inatoa nafasi kwa watu wa Turkana kupata maendeleo ikiwemo kuboreshwa kwa miundombinu, kuimarishwa kwa usalama na rasilimali za nyumbani. Ushirikiano huu umekuwa mtindo bora zaidi wa kutenga ardhi ya jamii kwa matumizi katika mradi huu muhimu wa kitaifa. Ninawaomba wadau wengine hasa waekezaji katika sekta za mafuta, kawi ya miale ya jua, upepo na mvunke wa ardhini kuiga mfumo huu wa kujipatia ardhi.

Ni matumaini yangu kwamba kuwepo kwa wanajeshi katika kaunti kutashughulikia changamoto za kila mara za ukosefu wa usalama katika mipaka yetu ya kimataifa na kuchangia maendeleo katika maeneo hayo.

Halmashauri ya ukusanyaji ushuru nayo pia imetengewa vipande vitatu vya ardhi huko Lodwar, Kainuk na Kakuma na Lomokori huko Lokiriama/Lorenggippi. Tunaiomba Halmashauri hiyo ya Ukusanyaji Ushuru kuharakisha ujenzi wa ofisi zao na kuweka vifaa ili kuimarisha usafirishaji wa watu na bidha na kuboresha biashara.

## **Wakaazi wenzangu,**

Katika Sekta ya Utalii, Utamaduni na Maliasili tumeweka utamaduni kama nguzo ya kuleta amani na muamko mpya miongoni mwa jamii za Waturkana na Ateker.

Tumeweza kuasisi Tamasha la Turkana la Utamaduni na Utalii linalojulikana kama Tobong'u Lore, huu ukiwa mradi wetu mkuu wa kukuza Amani ya Kikanda, Diplomasia, Biashara, Utamaduni na Maendeleo. Jamii ya Waturkana waliosoma sasa inatambua utamaduni wao Zaidi huku wakijihusisha kikamilifu na shughuli za kitamaduni.

Kufikia sasa tumeweza kuandaa awamu sita za Tamasha la Utalii na Utamaduni, linalojulikana kama Tobong'u Lore, ambalo lilihudhuriwa na wajumbe kutoka Uganda, Sudan Kusini na Ethiopia pamoja na wageni kutoka kote nchini Kenya. Ni matumaini yangu kwamba Gavana atakayeingia muhula ujao ataendeleza

tamasha hili ili kuboresha utalii, kuinua uchumi na kudumisha malengo ya amani na maendeleo kwa manufaa, sio tu ya watu wa Turkana bali kwa eneo zima.

Hatuwezi kuusahau umuhimu wa utamaduni katika kudumisha amani na maendeleo. Kuadhimishwa kwa mikataba ya amani ya Ata Nayece na Lokiriama kumewezesha muingiliano wa kijumuia na kupatikana kwa rasilimali za nchi jirani katika eneo hili. Hii imewezesha utangamano na ustawi katika mipaka ya Kenya, Uganda, Sudan Kusini na Ethiopia. Tukio hili linahitaji kuungwa mkono na kuendelezwa ili liweze kuzaa matunda zaidi

Ushirikiano wetu na Serikali ya Kitaifa kupitia Mpango wa Ushanga, umefaidi washonaji shanga 330 ambao wamepewa mafunzo ya ushonaji ulioboreshwa. Utawala wangu umetoa vifaa vya ushonaji kwa kina mama na vijana waliopewa mafunzo hayo ili kuboresha bidhaa wanazoshona. Hii imawaletea kina mama na vijana hao kipato mfukoni.

### **Mabibi na Mabwana,**

Ili kuboresha viwango vya misitu, juhudi zaidi zinahitajika kufanywa kuongeza maeneo ya misitu kufikia asilimia 10 iliyopendekezwa. Kutokana na hayo, utawala wangu umebuni nasari za miche ya miti katika Wadi za Lapur, Kibish, Kakuma, Turkwel, Kanamkemer, Lodwar Township, Lokichar na Lokori/Kochodin. Bado kuna kazi ambayo inahitaji kufanywa ili kuongeza eneo la misitu kufikia kiwango kinachohitajika cha asilimia 10. Hii inahitaji ushirikiano kati ya serikali, wadau na wakaazi ili kuhimiza desturi ya upanzi wa miti na kukomesha ukataji miti.

Tangu mwaka 2015, tumefanya kaguzi 468 za kimazingira, na kuwachukulia hatua wafanyibishara wasiotimiza kanuni. Kaguzi hizo zimefanyiwa viwanja vya mafuta huko Kusini mwa Turkana, Ujenzi wa Barabara na chimbo za mawe na mchnga miongoni mwa nyingine.

Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Utawala wangu unatekeleza Sheria ya Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ya Kaunti ya Turkana ya mwaka 2021.

Mchakato wa kubuni Hazina ya Kukabiliana na Tabianchi Kaunti ya Turkana unaendelea na utaziwezesha Kamati za Wadi 30 zilizopewa jukumu la kutekeleza mikakati ya kubaniliana na mabadiliko ya tabianchi katika ngazi za wadi.

Kaunti yetu sasa imetimiza asilimia 100 ya masharti ya mpango wa Ufadhili wa Benki ya Dunia juu ya hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Sheria hiyo inatoa nafasi ya kujumuishwa kwa mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya kisekta.

### **Wakaazi wenzangu,**

Kufikia leo hii, kazi ya kuweka taa za kawi ya miale ya jua imeendelea. Utawala

wangu umeweka taa za barabarani katika maeneo 13 ya miji mikubwa na vituo vya kibiashara mjini Lodwar, Kalokol, Kakuma, Lokichoggio, Oropoi, Lokichar, Lokori, Katilu, Kapedo, Kaeris, Lokitaung, Lowoarengak, na Kaaleng/Kaikor. Taa hizo za barabarani zimeimarisha usalama, kuboresha uchumi na kuongeza mapato kwa biashara na ukusanyaji ushuru

### **Mabibi na Mabwana,**

Ili kukuza uwezo wa sekta ya uchimbaji madini, kaunti hii imewasaidia wachimbani madini wa kibinafsi kubuni vikundi ili kurahisisha utoaji usaidizi kutoka kwa serikali na washirika wake.

Serikali yangu imesaidia kubuniwa kwa vyama vya kibiashara kwa wachimba migodi ambao sasa wamesajiliwa chini ya Chama cha Wachimba Migodi Kaunti ya Turkana ambacho kufikia sasa kina wanachama 23 ambao wanafadhiliwa na kamati ya Wachimba Migodi ya Kaunti ya Turkana. Kamati hiyo inasimamia utoaji leseni kwa migodi kote katika kaunti na kusaidia kutoa muongozo wa matumizi bora ya ardhi.

### **Wakaazi Wenzangu,**

Katika Sekta ya Utoshelevu wa Chakula na Lishe tumeongeza kiwango cha ardhi inayokuzwa mazao kimeongezeka kutoka ekari 8,900 mwaka 2013 hadi ekari 51,000. Hii imeongeza kiwango cha mazao ya kila mwaka hadi Tani 82.1 kutoka Tano 38.8. za mahindi na mtama.

Tumeanzia mifumo 51 ya kilimo cha umwagiliaji katika eneo la jumla ya ekari 16,176 inayonufaisha familia 27,485.

Ili kuwajengea uwezo wa uzalishaji wa kilimo watu wetu, wakulima 6,500 na vijana 40 wamepewa mafunzo ya kilimobiashara, lishebiashara na kilimo kinachotunza mazingira. Wakulima wengine 5,600 wamepewa mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya kuboresha mavuno ya mimea.

Serikali ya Kaunti imewekeza katika kilimo cha kutumia mashine ili kuboresha uzalishaji. Kufikia sasa tunazo Tingatinga 13 zinazowasaidia wakulima kutayarisha ardhi kwa upanzi. Mashine hizi zimepelekwa katika kaunti ndogo. Wakulima wamesaidiwa na pembejeo za kilimo zikiwemo tani 65.4 za mbegu zilizotolewa na serikali ya kaunti ya Turkana ikilinganishwa na tani moja iliyotolewa na serikali ya kitaifa mwaka 2013.

Utawala wangu umeshirikiana na Mpango wa Ufadhili wa Ugatuzi kujenga kituo cha mafunzo ya kilimo huko Naotin kwa gharama ya Shilingi Milioni 72. Ili kuimarisha uzalishaji tumeanza matumizi ya teknolojia bunifu ikiwemo kilimo cha umwagiliaji wa mafuriko na matone katika maeneo ya Lokwalia, Kachoda na Nakot. Zaidi ya Hekta 800 za ardhi ziko chini ya kilimo cha umwagiliaji na Hekta 280 zikiwa chini ya kulimo kinachotumia maji ya mvua yaliyotegwa na teknolojia za usimamizi katika maeneo ya Lomidat, Kakongu, Kajukjuk,

Lochoremeyan, Naroebai, Nawantos, Nakimomet, Kibish, Kalamng'orok, Nasinyono, Loupwala, Urum, Natiir, Kalopusia, Loya, Ng'isurumanyang, Nakalei, Loyal, Lokamarinyang, Nadunga, Kalemngorok, Naipa na Nadunga.

Tumeungana na Mpango wa Ufadhili wa Ugatuzi nchini kuanzisha kituo cha mafunzo huko Naotin kwa gharama ya awali ya Shilingi Milioni 72. Ujenzi wa kituo hicho unanza mwezi huu huku mwanakandarasi akikabidhiwa mradi huo.

Ili kujenga ujuzi wa kiufundi unaohitajika kuweza kutimiza malengo ya utoshelevu wa chakula, serikali ya kaunti kupitia msaada wa kiufundi kutoka Ubalozzi wa Israeli mwaka uliopita iliwapa wanafunzi wanane wa kilimo kutoka Turkana msaada wa masomo kwenda nchini Israel kujifunza.

Wanafunzi wengine 10 watajiunga na kundi la kwanza nchini Israel kwa mafunzo hayo.

### **Mabibi na mabwana,**

Uchumi wa ufugaji umebaki kuwa nguzo ya kiuchumi ya uchumi wa Kaunti yetu na ambao haujatumiwa kikamilifu huku ngombe 247,145, mbuzi 2,429,224, ngamia 237,237 na punda 93,816 wakisimamia Maisha ya asilimia 80 ya idadi ya watu katika kaunti.

Utawala wangu umeweka msingi ambao unafunguo uwezo wa ufugaji wa kuhamahama kwa lengo la kuondokea ufugaji wa matumizi ya chakula hadi ufugaji wa kibiashara.

Tumewekeza katika miradi ya ustawi wa miundombinu ambayo ni Pamoja na Maabara ya Mifugo mjini Lodwar, majokovu matatu mjini Lodwar, Lokitaung' na Lokichar; vizimba 21 vya kuhamishwa vya ngo'mbe, vituo vya uzalishaji mifugo huko Lomosogol, Wadi ya Kerio na uwanja wa kuzuilia mifugo katika eneo la Napeililim.

Ili kuboresha urahisi wa kufikia masoko, tumejenga masoko 18 ya mifugo na kufikisha jumla ya idadi ya masoko kuwa 38 kwa wakati huu na hivyo kuwafaidi watu 240,000

Tumejenga mabohari ya kuhifadhi lishe ya mifugo huko Kakuma, Lokichar, Kanamkemer, na Kaaleng/Kaikor kuhifadhi lishe inayotumika wakati wa msimu wa kiangazi. Lishe hiyo husambazwa kupitia hifadhi kuu ya lishe iliyoko Lodwar iliyo na uwezo wa kuwanufaisha takriban wafugaji 10,000.

Tumeongeza idadi ya maafisa wetu wa mifugo. Idadi ya Madktari wa mifugo katika kaunti imeongezeka kutoka Madktari watano mwaka 2013 hadi 15 wakati huu, Wahudumu wa Afya ya Mifugo nao wamkiongezeka kutoka saba mwaka

2013 hadi 14 wakati huu, huku kauti hii ikiwa wanateknolojia 4 wa Mifugo ambapo kaunti hii haikuwa na hata mmoja mwaka 2013.

Pia tumeongeza maripota wa magonjwa ya mifugo katika jamii kutoka 87 mwaka 2013 hadi 297 wakati huu. Maripota hao ni muhimu katika kutambua na kuzuia magonjwa ya mifugo.

Juhudi hizi Pamoja na ushirikiano ambao umewezesha usambazaji wa dawa za mifugo na kuongeza idadi ya mifugo waliochanjwa kutoka asilimia 20 hadi asilimia 50 kufikia sasa.

Ili kuwafidia wafugaji dhidi ya hasara ya kupoteza mifugo kutokana na ukame na ukosefu wa usalama, utawala wangu umeanzisha shughuli ya kurejesha mifugo katika Wadi zilizoathiriwa zikiwemo Kaputir, Lobokat, Kapedo/Napeitom, Lokori/Kochodin, Katilia, Kerio Delta na Turkwel.

Katika Sekta ya Uvuvi tumepiga hatua ya kuwasaidia wavuvi. Tumetoa neti alfu 17 kwa vituo 25 vya wavuvi na mashua 28 za fibreglass kwa wavuvi 56 wanaotumia ngalawa kutoka Kalokol, Kangatotha na Kerio.

Utawala wangu uko katika harakati za kununua mashua 200 zinazotengezwa na mafundi wetu wenyewe. Kufikia sasa mashua 50 za Wadi ya Lakezone ziliwasilishwa kwa vituo 15 vya usimamizi wa fuo za ziwa na makundi 15 ya vijana na kina mama. Zaidi ya hayo, Boti 3 za Fibreglass zitakazotumika kushika doria za usalama na uokoaji zimewasilishwa na kwa wakati huu zinasimamiwa na idara ya uvuvi Kaunti ya Turkana.

Ili kuimarisha biashara ya samaki na soko lake, kaunti imejenga masoko matatu ya Samaki wa kukaushwa huko Lowarengak, Nachukui na Kerio na kujengwa kwa majukwaa matano ya kukaushia Samaki katika Kisiwa cha Choro na Kaitio.

Kwenye ripoti iliyozinduliwa mwezi uliopita kuhusu tathmini ya kiuchumi katika Ziwa Turkana iliyofanywa na Ubalozi wa Uholanzi, uzalishaji wetu wa Samaki unakadiriwa kuwa tani 16,100 ambao una uwezo wa kuingiza Shilingi Bilioni 5.3 katika uchumi wetu. Tumejitolea kuweka majokovu Zaidi kandokando mwa ziwa Turkana ili kuimarisha soko la Samaki, kutumia mbinu endelevu za uvuvi na matumizi bora ya rasilimali za ziwa.

### **Wakenya Wenzangu,**

Tumepiga hatua kubwa katika kukabiliana na ukosefu wa usalama. Kabla nishike hatamu za uongozi mizozo ya kuzozania rasilimali miongoni mwa makundi ya wafugaji ilikuwa imekithiri ndani na kwenye mipaka yan chi Jirani, Kwa kutambua kwamba Amani na kigezo cha maendeleo, utawala wangu unatambua hilo. Serikali yangu imewekeza kwa kiasi kikubwa katika juhudi za kujenga amani na mipango ya usimamizi wa mizozo na kubuni ofisi ya kushirikisha mipango hiyo.

Maadhimisho ya Mkataba wa Amani wa Lokiriyama, Kumbukumbu ya Ata Nayece na Tamasha la Kitamaduni la Tobong'u Lore, imesaidia kutuliza maeneo ambayo awali yalikuwa na uhasama. Kujitolea kwetu kuwa msitari wa mbele katika michakato ya amani ya kieneo huku utawala wangu ukishiriki katika mazungumzo ya ushirikiano wa kiserikali na Wilaya za Karamoja nchini Uganda, Equatoria Mashariki ya Sudan Kusini na Omo Kusini nchini Ethiopia kumbainika na kudumushishwa. Juhudi hizi ndizo zilizopelekea kutiwa Saini kwa Mwafaka wa Makubaliano kuhusu Amani na Maendeleo kati ya Kenya na Uganda mwaka 2019. Mkataba huo umelenga kuleta amani na ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa

kwa Turkana, Pokot Magharibi na Wilaya za Karamoja nchini Uganda.

Baadhi ya manufaa ya mkataba huo ni Pamoja na kuimarika kwa biashara ya mpakani kati ya Lodwar na Moroto, urahisi kwa wafugaji kupata maji na lishe, ambapo nyakati za kiangazi wamekuwa wakihamia nchini Uganda. Ninatarajia kwamba serikali za Kenya na Uganda kwa ushirikiano na serikali za kaunti zitaharakisha kuratibiwa rasmi kwa mkataba huo wa miaka 10 wa amani na mpango wa maendeleo ili matunda yake yaweze kuonekana kwa raia wa wananchi

Ninatambua kikamilifu juhudi za washirika wetu wa kimaendeleo ambazo zinachangia amani na maendeleo katika maeneo yanayokabiliwa na mizozo.

Ili kushughulikia swala la wakimbizi wa ndani kwa ndani ambao ni waathiriwa wa wizi wa mifugo na uvamizi wa ardhi, serikali yangu imewapa hifadhi familia 520 katika kambi za Kasarani, Kakiteitei, Nadome, Lomoro na Kapedokatika Wadi ya Kapedo/Napeitom, Naakot na Namambu huko Lobokat; Kaloporor katika Wadi ya Kalapata; Kachalang'a, Kangipetain huko Lokori/Kochodin; Lodwat huko Lokoriyama/Lorenggipin; Loteteleit huko Lokichoggio; Lokaabuk huko Kalabeyei; Loruth sehemu ya Kaleng/Kaikor; Liwan huko Lapur, Todonyang A na B huko Lakezone; Makutano ya Natodomeri na Napus, kambi za Kibish; Kapetadie huko Nanm na Nakitong'o katika wadi ya Letea.

Katika siku za usoni kuna haja ya kupanua mpango wa kuwapa makao wakimbizi hadi maeneo mengine yaliyoathiriwa ikiwa ni Pamoja na Koolok huko Katilu, Nariwomoru huko Kaputir, Lomokori na Kaemanic huko Lokiriyama/Lorenggipi. Kupanuliwa hadi Nadome na Kasarani huko Kapedo na Nnam; Namambu na Naakot huko Lobokat.

Ili kubuni mifumo ya usuluhishaji mizozo, usimamizi na kujenga amani Mswaada wa Kutafuta Amani wa Kaunti ya Turkana mwaka 2022 unajadiliwa katika Bunge la Kaunti. Nalihimiza Bunge hilo kuidhinishwa mswaada huo kambla mwishoni mwa muhula wake.

**Mabibi na Mabwana,**

Ufanisi mkubwa umepatikana Katika Sekta ya huduma kwa Umma, Utawala na Usimamizi wa Majanga. Idadi ya wafanyikazi wa kaunti saa hii inafikia watu 3,698 wanaotoa huduma katika sekta mbali mbali. Huku hii ikionekana kuwa ufanisi, kuna haja ya kuajiri maafisa zaidi wa kiufundi katika maeneo maalumwakiwemo maafisa wa afya waliosomea taaluma spesheli, wauguzi, madaktari, wataalam katika sekta za ujenzi wa miundombinu, wataalam wa majabali na maji na walimu wa chekechea miongoni mwa wengine. Hivi majuzi, utawala wangu ulifanya ukaguzi wa Wafanyikazi ili kujua ni wafanyikazi wangapi na ni huduma zipi wanazotoa. Matokeo na mapendekezo yake yatatekelezwa ili kulainisha utoaji huduma.

Sasa tunayo Sheria ya Kaunti ya Turkana ya mwaka 2019 ya Utawala wa Vijiji ambayo inagatua mifumo ya serikali hadi sehemu ya chini ya utawala kufikia ngazi ya Kijiji. Maafisa 155 wa vijiji tayari wameajiriwa na kupelekwa katika vitengo vya vijijini.

Shughuli ya kuwateua wanachama 780 wa baraza la vijiji inaendelea na watakapoteuliwa wanatarajiwa kuongeza ushiriki wa raia katika mipango ya serikali.

### **Mabibi na Mabwana,**

Katika juhudi za kukabiliana na ukame, utawala wangu umetumia jumla ya shilingi Bilioni 3.7 na kununua tani 44,414.2 za bidhaa za vyakula ambazo zinawanufaisha watu laki sita kila mwaka.

Ukame ulitangazwa kuwa janga la kitaifa mnamo tarehe 8 mwezi Septemba mwaka 2021 na Rais Uhuru Kenyatta. Hata hivyo juhudi za serikali ya kitaifa za kukabiliana na athari za ukame huo zimekuwa haba na hii inatia wasiwasi.

Ili kukabiliana na uhaba uliopo wa chakula, serikali yangu inanunua tani 2, 500 za bidhaa aina mbali mbali za vyakula ili kusambazwa punde tu kiwango kitakapokusanywa cha kutosha.

Ningependa kuwapongeza washirika wetu wanaofanya kazi katika Kaunti katika juhudi zao za kusaidia mikakati ya kukabiliana na ukame na mipango ya kutoa pesa kwa waathiriwa ili kuendeleza mpango huo.

Kama sehemu ya kutekeleza Sheria ya Mwaka 2016 ya Kushughulikia Dharura na Usimamizi wa Mikasa ya Kaunti ya Turkana, tumeanzisha kamati 11 za Usimamizi wa Mikasa ya Dharura. Kituo cha Kaunti cha Shughuli za Dharura kinasaidia ukusanyaji Habari na hatua za dharura zinazohusiana na majanga katika kaunti. Ninatoa mwito kwa washirika wetu kusaidia kuimarisha kituo hicho kama sehemu ya mfumo wa tahadhari ya mapema. Kituo hicho kinasaidia ukusanyaji Habari kuhusiana na Mikasa katika Kaunti. Ningependa kutoa wito kwa washirika kusaidia kuimarisha kituo hicho kwama kiungo cha tahadhari za mapema

## **Wakaazi wenzangu,**

Hatua pia imepigwa katika Sekta ya Biashara, Jinsia na Maswala ya Vijana. Ili kuhimiza biashara katika kaunti, serikali yangu imejenga masoko 16 mapya ya kisasa katika miji na vituo vya kibishara vya Lokitaung', Lodwar, Lokiriana, Kakuma, Towokayen, Natukobenyo, Tumaini, Kalokol, Nakurio, Loya, Turkwel, Lokori, Lokichar. Hili ni ongezeko kubwa kutoka masoko mawili mwaka 2013.

Kufuatia kubuniwa kwa sheria ya mwaka 2015 ya Hazina ya Biashara ya Kaunti, mwezi Machi mwaka huu nilizindua utoaji wa Shilingi Milioni 185 kwa Biashara 3,000 ndogongo na za kadri kote katika kaunti.

Hazina hii itawasaidia wafanyibiashara kupata mikopo ya riba ya chini na kuhimiza uwekezaji wa ndani ya kaunti. Lengo kuu ni kukuza hazina hii iwe chanzo cha kimsingi cha mikopo kwa wafanyiniashara kutoka ndani ya Kaunti ya Turkana. Kwa hiyo chaguo lenu la utawala hasa mtu mtakayemchagua kuchukua nafasi yangu itakuwa ni jambo la muhimu katika kuhakikisha mpango huu unaendelezwa.

Nina furaha kuripoti kwamba idadi ya leseni za biashara imeongezeka hadi 7,300 wakati huu. Kutoka 2100 mwaka 2013. Ongezeko hili ni dalili ya ukuaji wa kibiashara na umeongeza kiwango cha ushuru kwa serikali ya kaunti.

Kufikia sasa serikali yangu imewapa mafunzo wafanyibiashara 2000 wa biashara ndogongo na za kadri juu ya usimamizi wa biashara na elimu ya kiuchumi. Mafunzo hayo yalinuiwa kuyapa makundi hayo mbinu na ujuzi wa usimamizi ili kuongeza faida kwa biashara zao.

Vituo viwili vya Biashara mjini Lodwar na Kakuma vinakaribia kukamilika. Vitakapokamilika vituo hivyo vitatoa huduma za ustawi wa bishara na mafunzo kwa vijana, wanawake na Walemavu. Kituo cha Kakuma kitatoa huduma zote za serikali kusaidia jamii ya kibiashara na umma.

Katika juhudi za kuimarisha ustawi wa ushirika, serikali yangu imesajili vyama vipya vya ushirika 51 kutoka vyama 33 mwaka 2013. Vyama vya ushirika vya akiba na mikopo vimewezesha wanachama kuweka akiba na kupata mikopo na nafasi ya kuuza mazao yao kwa Pamoja.

Mabibi na Mabwana,

Katika Sekta ya Miundombinu, Usafiri na Ujenzi, utawala wangu kwa kushirikiana na Halmashari ya Barabara Nchini kupitia Hazina ya Ushuru wa Barabara tumejenga na kukarabati kilomita 12,000 za barabara za Maram kote katika kauti kwa gharama ya Shilingi Bilioni 1.7. tumejenga kilomita 10 za barabara za lami ndani ya Manispaa ya Lodwar. Ili kuimarisha usalama, tumejenga barabara za mashinani zifuatazo, Kibish na Turkana Mashariki;

Lokoru Kamuge, Ngilukia-Kangibilae-Parkati, Kibish-Dume, Lokwamosing-Lochakula miongozi mwa nyingine.

Ili kuhakikisha utoaji huduma, usafiri wa bidhaa na huduma kwa watu wa Kaunti ya Turkana, tumejenga madaraja ya mafuriko 31kote katika Kaunti ikiwemo Lopeduru ambalo ndilo refu Zaidi katika Wadi ya Katilia.

Tumejenga madaraja mawili; Daraja la Nawoyaregae huko Kaputir linalohudumia watu 50,000 na lile la Kotome huko Kaikor/Kaaleng linalohudumia watu 24,000.

Kwa wakati huu Manispaa ya Lodwar inafanyiwa ambao ni Pamoja na ujenzi wa vibanda vya soko katika sehemu ya Kamamkemer, na taa kubwa za ulinzi katika mji wa Kanamkemer, ujenzi wa vyoo vya umma katika Kambi Mawe, Kambi Moto na Nadiirkonyen, kuhamishwa kwatika eneo la Nayanaeangikalalio mjini humo, kufanyiwa ukarabati Msitu wa Lodwa mjini na urembeshaji wa mji wa Lodwar.

Kupitia Uwajibikaji wa Kijamii wa Mashirika Miradi iliyoanzishwa kupitia akiba za kodi ya barabara za kiwango cha A1, Shirika la Barabara Kuu nchini Kenya KeNHA na serikali ya kaunti ya Turkana itaweka Bilioni 2.8 kwa ustawi wa miundombinu Kauti ya Turkana. Miradi hiyo inayojumuisha mabomba ya maji, kujenga shule za kisasa za msingi na sekondari, Hospitali na Masoko inafanyiwa utaratibu wa kutolewa zabuni. Miradi hiyo inasimamiwa na KeNHA na timu ya Pamoja ya shirika hilo na Kaunti litasimamia ujenzi wa miradi hiyo. Utawala wangu umekamilisha kazi ya kukinga mito Lokichar na Lokichoggio ambayo inasaidia kuzuia mafuriko wakati wa mvua nyingi. Tumetoa mwito kwa KeNHA kujumuisha mito ya Kainuk, Kawalase na Turkwel iweze kushirikishwa katika ujenzi wa kingo zake kwani haiwezi kujumuishwa katika mpango wa Uwajibikaji wa Kijamii wa Mashirika kwa barabara kuu ya A1 na bado ninafuatilia.

Mwezi uliopita Pamoja na Halmashauri ya kitaifa ya Usalama wa Usafiri NTSA nilibuni kamati ya Usalama kusimamia maswala yanayoathiri usafiri. Mwenyekiti wa kamati hiini Mwanachama wa Kamati Kuu ya Kaunti anayesimamia Uchukuzi. Kamati ina jukumu la kusimamia usafiri katika kaunti Pamoja na taa barabarani, sehemu za kuegesha magari na barabara za umma miongoni mwa majukumu mengine.

Wakaazi wenzangu,

Katika sekta ya Elimu, Michezo na Ulinzi wa Jamii, ambako tuna changamo kadhaa za viwango vya juu vya kutojua kusoma na kuandika, ukosefu wa kujiunga na shule na ukosefu wa ujuzi, tumepiga hatua katika masomo ya chekechea na kiufundi kwa kutoa karo kwa wanafunzi wa shule za upili na vyuo.

Katika elimu ya Chekechea, utawala wangu umejenga vituo 243 ambavyo vitaongeza vituo vya elimu ya Chekeche kufikia 937.

Leo hii idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa kujiunga na masomo ni 137,000; wavulana wakiwa 71,000 na washichana 66,000. Idadi ya walimu waliopata mafunzo ya kufunza chekechea pia imeongezeka hadi 570 tangu mwaka 2013..

Ili kuhakikisha wanafunzi wanabaki katika vituo hivyo, Serikali ya Kaunti kwa ushirikiano na wadau wa kimaendeleo imeanzisha mpango wa lishe ambapo kila mwaka tunatenga Shilingi Milioni 130 kusambaza vyakula aina mbali mbali katika vituo cha Chekechea, hatua ambayo tunakadiria kwamba imechangia asilimia 76 ya wanafunzi kubaki shuleni.

Idadi ya vyuo vya Kiufundi imeongezeka kutoka viwili mwaka 2013 hadi vinane wakati huu. Vituo hivyo ni Lodwar, Kalokol, Lokichoggio, Kataboi, Lorugum, Kaelang, Lokori na Lokichar. Vituo hivyo vinawapa vijana katika kaunti nafasi ya kujipatia maarifa na ujuzi muhimu ya kukidhi mahitaji ya ajira. Usajili wa wanafunzi katika vyuo hivi umeongezeka kutoka 100 mwaka 2016 hadi 2,000 wakati huu. Idadi ya wakufunzi nayo imeongezeka hadi 80 kutoka 24 awali.

Miaka sita iliyopita serikali yangu ilizindua Mpango wa Kuboresha ujuzi kusaidia wanafunzi wanaojiunga na shule za sekondari na vyuo vya masomo ya juu. Tangu wakati huo serikali ya Kaunti imetoa shilingi Bilioni 1,9 kwa Zaidi ya wanafunzi 212,000 katika ngazi mbali mbali za kielimu.

Mkakati wa Ulinzi wa Watoto ulioanza kutekelewa mwaka 2019 ni mfumo wa ushirikishi kati ya serikali na wadau kutoa ulinzi kwa Watoto.

Utawala wangu umeanzisha vituo viwili vya kuwanusuru watoto katika miji ya Kamuma na Lodwar Vituo hivi vinatoa msaada wa matunzo kwa watoto walio katika hatari ya kutelekezwa. Tangu mwezi Julai mwaka 2020, jumla ya Watoto 98 wamenusuriwa katika kituo cha Lodwar. Kati ya hao 58(Wavulana 39 na Wasichana 19) wameunganishwa na familia zao.

Kuna haja ya vituo Zaidi kubuniwa katika sehemu za miji ili kuendeleza ulinzi dhidi ya dhuluma na utelekezaji wa watoto.

### **Wakaazi wenzangu,**

Utawala wangu umeongeza uwekezaji kuhakikisha ushirikishi wa vijana katika michezo huku tukibuni nafasi kwa ustawi wa talanta. Hii ni Pamoja na msaada kupitia usambazaji wa vifaa vya michezo, ufadhili wa kushiriki katika mashindano ya kieneo na kimataifa. Mashindano kama hayo ni pamoja na yale ya kila mwaka baina ya kaunti yanayoandaliwa na Chama cha Michezo cha Vijana Nchini Kenya, mashindano ya walemavu ya kuendesha viti vya magurudumu nyikani, masumbwi, mbio za nyika na mashindano ya Karate. Pia tumesaidia walemavu kushiriki katika mashindano yakiwemo yale ya

mwaka jana ya kandanda, mashindano baina ya Kaunti ya Viziwi yaliyofanyika mjini Nakuru na mashindano ya Voleboli yaliyofanyika katika uwanja wa Nyayo mjini Nairobi, mashindano ya Mpira wa Vikapu kwa viziwi yaliyofanyika Nairobi na mashindano ya riadha yaliyofanyika Nairobi vilevile.

Nina furaha kukariri kwamba wanariadha wetu wameshiriki kwenye mbio za baiskeli za viti kwa magurudumu tangu mwaka 2013.

Tangu awamu yake ya kwanza mwaka 2018, Mbio za nyika za Tobong'u Lore zimeimarika huku wanariadha tajika katika kanda hii wakishiriki. Kila mwaka wanariadha chipukizi hupata fursa ya kushindana na wakimbiaji magwiji huku tukizifanya mbio hizo kuwa sehemu ya kalenda ya mashindano ya riadha ya kila mwaka.

Kuanzishwa kwa miundimsingi ya michezo ni muhimu katika kufadhili michezo. Michoro ya uwanja wa kisasa wa michezo uliopangwa kujengwa mjini Lodwar imekamilika na ujenzi wa uwanja huo unakadiriwa kugharimu Shilingi Bilioni 2.7. Uwanja huo utakaokuwa na uwezo wa kuketi watu alfu 20 utakuwa ngome ya michezo na ustawi wa talanta na utaturuhusu kuandaa mashindano ya kitaifa ya michezo mbali mbali.

Uwanja wa michezo wa Kakuma/Kalobeyi ambao ujenzi wake ulifadhiliwa na Shirika la Wakimbizi UNHCR umekamilika na uko tayari kukabidhiwa serikali ya Kaunti. Uwanja huo utaimarisha mipango ya utangamano wa jamii za wakimbizi na wenyeji.

### **Wakaazi wenzangu,**

Katika sekta ya Fedha na Mipango ya kiuchumi, jumla ya fedha za maendeleo tulizopokea kutoka kwa hazina kuu ya serikali ya kitaifa katika kipindi cha fedha FY13/14 hadi FY 21/22 ni shilingi Bilioni 154.25(Sh Bilioni 95.5 kutoka serikali kuu na Sh Bilioni 58.5 kutoka kwa washirika wetu wa kimaendeleo) dhidi ya nakisi ya rasilimali ya Shilingi Bilioni 143.1 zilizonuiwa kufadhili kikamilifu CIDP I na CIDP II ambayo ni asilimia 48 ya rasilimali zilizohitajika. Katika kipindi saw ana hicho, mapato yetu ya jumla kutoka kwa ushuru tunaotoza ni Shilingi Bilioni 1.385 dhidi ya shabaha yetu ya Shilingi Bilioni 1.48 hiyo ikiwa ni asilimia 94 ya utendajikazi. Washirika wetu wa kimaendeleo yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali, Umoja wa Mataifa na Mashirika ya kijamii yamechangia shilingi Bilioni 58 kes kipindi cha **fedha cha mwaka 2013/2014** hadi sasa. Hata hivyo shilingi Bilioni 44 ziliwekezwa kuboresha viwango na hali ya Maisha ya wakimbizi katika kambi ya Kakuma/Kalobeyi. Huku shilingi Bilioni 14 zikinufaisha Jamii ya Turkana.

Kutokana na kupandana kwa utekelezaji wa miradi na kuchelewa kutolewa kwa fedha kutoka serikali kuu katika kipindi cha matumizi ya fedha za serikali

mwaka uliopita, Kaunti ililimbikiza madeni ya shilingi Milioni 417. Tayari tumelipa Shilingi Milioni 313 ambazo ni asilimia 75 ya jumla ya madeni ambayo hayakuwa yamelipwa.

Tungependa kukariri nia yetu na kujitolea kwetu kuhakikisha madeni yote yaliyosalia yanalipwa kufikia mwisho wa kipindi cha matumizi ya serikali mwaka huu. Hata hivyo ni sharti zitimize kanuni ziwe zina ukweli na kuambatana na stakabadhi muhimu zinazoonyesha hitaji la malipo. Serikali yangu itawasilisha katika ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu madeni yote ya jumla ya Shilingi Bilioni 3 kufanyiwa uchunguzi na kuidhinishwa ili malipo yaweze kufanyika.

### **Wakaazi wenzangu**

Ninapohitimisha kipindi changu cha uongozi kinakamilika baada ya uchaguzi mkuu wa tarehe tisa mwezi Agosti na kuapishwa kwa Gavana mpya kuchukua hatamu za uongozi, ningependa kusema kwamba ninayo ninajivunia rekodi ya maendeleo na msingi ambao nimeuacha nyuma. Ni matumaini yangu kwamba utawala ujao utasukuma mbele ufanisi tuliopata.

Ni kutokana na uwekezaji wa hatua kwa hatua wa Serikali ya Kaunti **na** washirika wetu wa kimaendeleo tumeweza kubadili sura ya Turkana. Miradi ya maendeleo katika sekta zote imesambaa kote katika kaunti, hiyo ikimaanisha kwamba serikali ijayo ya kaunti itarithi msingi thabiti wa kueleza maendeleo hayo. Mpango Shirikishi wa Maendeleo wa Kalobeyei ulioanza kutekelwa mwaka 2016 unanua kuboresha hali ya kiuchumi na kijamii ya wakimbizi na Jamii za wenyeji wa Turkana Magharibi. Jumla ya hitaji la mradi huo lilikuwa Shilingi Bilioni 58 na kufikia sasa utekelezaji wake kutoka kwa washirika wa kimaendeleo ulifika shilingi Bilioni 12.5

Mradi wa KISDEP umeanzisha Chumba cha Watoto na Hospitali ya Ammusait huko Kakuma, Kituo cha Elimu cha Turkana Magharibi, Kituo cha elimu ya juu kinachojumuisha mafunzo kwa walimu na Shule ya Mabweni ya wasichana huko Kalobeyei.

Mpango huo kupitia Shirika la Makaazi la UN Habitat ulifadhili mpango wa wa miundombinu kwa ujenzi wa Manispaa ya Kakuma/Kalobeyei.

Kuhusu utoshelevu wa chakula ushirika wetu umepata kujengewa Bwawa la Kangura lenye uwezo wa kuweka cubic mita 1000,000 za maji na Bwawa la Pelekech la Cubic Mita 50,000 kupitia ufadhili wa mashirika ya FAO na WFP. Pia tungependa kutambua ufadhili wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha mifugo uliofadhiliwa na Baraza la Makanisa NCKC

Pia tunajengewa mtandao wa internet utakaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Fedha IFC. Serikali ya Kaunti ya Turkana itakuwa na uwezo wa kuhifadhi takwimu za maendeleo kupitia mtandao huo.

Aafisa wetu wa serikali wakiwemo wa Biashara na Ufunzi wamepata mafunzo kuhusu mawasiliano ya kibiashara kwa ajili ya kuimarisha uwekezaji.

Shirika la Fedha la Kimataifa ambalo ni tawi la Benki ya Dunia linasaidia ujenzi wa kituo cha Huduma na Biashara mjini Kakuma.

Ni muhimu tujikumbushe ya kwamba licha ya juhudi ambazo tumeweka katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, changamoto bado tunazo. Lakini mbali na hayo kunazo nafasi nzuri ambazo hazijatumiwa kikamilifu ambazo zinaweza kutumiwa kukabiliana na ukosefu wa mapato na ajira, Juhudi kabambe zinahitaji kufanywa kulenga uwekezaji wa kinyumbani katika mifugo, uvuvi, kilimo cha umwagiliaji na biashara. Kama mkaazi wa Turkana na kiongozi wa kisiasa na mzee, ninajitolea kuendelea kuchangia juhudi hizi kutoka mahali popote nitakapokuwa.

Ni matumaini yangu kwamba wewe mpiga kura utamchagua Gavana aliye na maono, uwezo na kujitolea kuipeleka Turkana katika ngazi nyingine ya juu zaidi.

Ninaahidi kutoa ujuzi wangu kuhusu ufanishi na mapungufu tuliyoyashuhudia ili kuhakikisha utawala ujao unapata vifaa bora vya kuleta ufanisi.

Katika muda huu uliosalia wa utawala wangu na wakati wa kipindi hiki cha kampeni ambazo tayari zimeanza nawahakikishia kwamba utoaji huduma na utekelezaji wa miradi utaendelea hadi nitakapomkabidhi usukani Gavana atakayechukua nafasi yangu.

Ninaamini kwamba nimewahudumia kwa uadilifu na kwa juhudi kadri ya uwezo wangu. Asanteni kwa kunipa Imani yenu na kunichagua mara mbili kama Gavana wenu.

Kwa mara nyingine tena ningependa kuwatakia wakaazi wa Turkana Sikukuu ya Madaraka yenye furaha na kipindi cha amani cha kampeni na uchaguzi.

**Mungu awabariki, Mungu aibariki Turkana, Mungu aibariki Kenya!**





**Ee Mungu nguvu yetu  
Ilete baraka kwetu  
Haki iwe ngao na mlinzi  
Natukae na undugu  
Amani na uhuru  
Raha tupate na ustawi.**

**Amkeni ndugu zetu  
Tufanye sote bidii  
Nasi tujitoe kwa nguvu  
Nchi yetu ya Kenya  
Tunayoipenda  
Tuwe tayari kuilinda**

**Natujenge taifa letu  
Ee, ndio wajibu wetu  
Kenya istahili heshima  
Tuungane mikono  
Pamoja kazini  
Kila siku tuwe na shukrani**

**Ee Mungu twaomba ulinde  
Jumuiya Afrika Mashariki  
Tuwereshe kuishi kwa amani  
Tutimize na malengo yetu.**

**Jumiya Yetu sole tuilende  
Tuwajibike tuimarike  
Umoja wetuni nguzo yetu  
Idumu Jumuiya yetu.**

**Uzalendo pia mshikamano  
Viwe msingi wa Umoja wetu  
Natulinde Uhuru na Amani  
Mila zetu Na desturi zetu.**

**Viwandani na hata mashambani  
Tufanye kazi sote kwa makini  
Tujitoe kwa hali na mali  
Tuijenge Jumuiya bora.**